TANGAZO LA SERIKALI Na. 26 la Tarehe 17/1/2025

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))*

MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI YA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 39 la 2024

**1.** Sheria Ndogo hii itajulikana kama Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ya Mwaka 2024 ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya kifungu cha 8

**2.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kifungu cha 8(1) kwa-

(a) kufuta aya (b); na
(b) kubadili mpangilio wa aya (c) kuwa aya (b).

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

**3.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika Jedwali la Kwanza-

(a) katika aya ya 3 ya Sehemu ya Kwanza kwa kuongeza maneno "kwenye viwanja vya Halmashauri" mara baada ya neno "kandanda" lililopo katika safu ya pili ya kipengele cha 10; na
(b) kwa kuongeza maneno "MAMLAKA" kabla ya maneno "YA MAPATO" mwanzoni mwa kichwa cha habari cha Sehemu ya Kumi na Tatu.

Marekebisho ya Jedwali la Tatu

**4.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika Jedwali la Tatu kwa kufuta maneno "Mlimba" yaliyopo kwenye fomu ya Kibali cha Uchimbaji wa Madini ya Ujenzi na badala yake kuweka maneno "Moshi".

Dodoma,
25 Machi, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri Wa Nchi- OR-TAMISEMI*